

# HALMASHAURI YA MJI WA KONDOA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Halmashauri ya Mji wa KondoA)

Simu: +255 712264912

Nukushi: +255 262360313

Barua pepe: [td@kondoatc.go.tz](mailto:td@kondoatc.go.tz)

Tovuti: [www.kondoatc.go.tz](http://www.kondoatc.go.tz)



Mkurugenzi wa Mji

S.L.P 711,

KONDOA.

---

## TAARIFA YA IDARA YA MAENDELEO YA JAMII

### 1.0 UTANGULIZI

Idara ya Maendeleo ya Jamii ni moja ya idara 13 zilizopo ndani ya Halmashauri ya Mji KondoA. Idara hii inashirikiana vema na idara nyingine katika kutekeleza shughuli za maendeleo.

Idara ya Maendeleo ya Jamii inahamasisha ushirikishwaji wa jamii katika kazi za maendeleo ambayo ni hatua muhimu ya kuifanya jamii kuweza kujua miradi iliyopo katika maeneo yao na hivyo kuweza kushiriki ipasavyo katika utekelezaji wake.

Ushiriki wa Jamii kwenye utekelezaji wa kazi za maendeleo unaongeza ubunifu kwao na hivyo kuwafanya kuweza kutekeleza miradi mingine ya namna hiyo kwa kushirikiana na wataalam wa maendeleo ya Jamii walioko katika maeneo husika.

Miradi inayotekelezwa kwa kushirikiana na wanajamii inaongeza umiliki imara kwa jamii, wanailinda na kuitunza kwa kuwa ipo kwa manufaa yao wenyewe.

Kazi za maendeleo ni zile shughuli zote zinamsaidia mwanajamii kujipatia huduma za kijamii (elimu, afya, maji, barabara mazingira safi n.k)

Uhamasishaji wa Jamii unahitaji umakini wa kuwahusisha watu wa makundi yote katika jamii husika. Ushiriki wa makundi unasaidia

kuwezesha kufahamu mahitaji ya kila mmoja na hivyo kusaidia kuboresha hali za kila mmoja na kupata ufumbuzi muafaka.

## **2.0 MAWASILIANO YA WATUMISHI WA IDARA YA ELIMU MSINGI**

Idara ya Maendeleo ya Jamii ina Jumla ya watumishi watatu na mawasiliano yao ni kama inavyoonekana kwenye jedwali:-

<b>SN</b>	<b>JINA LA AFISA</b>	<b>CHEO</b>	<b>NAMBA YA SIMU</b>
1.	Robert Sungura	Afisa Maendeleo ya Jamii	
2.	Ally Mwinyikombo	Afisa Maendeleo ya Jamii	0719099171
3.	Latipha Koshuma	Afisa Maendeleo ya Jamii	0684 459519

## **2.0 KAZI ZA IDARA**

Idara inatekeleza majukumu mbalimbali kama ifuatavyo;

- I. Kuhamasisha jamii kushiriki katika shughuli za Maendeleo
- II. Kuwezesha uingizaji wa masuala ya Jinsia katika mipango ya Halmashauri
- III. Kuandaa na kusimamia mafunzo ya viongozi wa vijiji na vikundi mbalimbali vya maendeleo katika halmashauri
- IV. Kueneza elimu ya uraia
- V. Kuhamasisha jamii kujiunga katika vikundi vidogo vidogo
- VI. Kuratibu usajili wa vikundi vya uzalishaji mali
- VII. Kukusanya taarifa muhimu kuhusu masuala mtambuka kama vile UKIMWI na mila zenye madhara kwa wanawake na watoto wa kike

- VIII. Kuratibu na kuhamasisha jamii kujiunga na mfuko wa afya ya jamii (CHF)
- IX. Kuratibu shughuli za maendeleo kwa kuzingatia jinsia
- X. Kuhamasisha na kuratibu shughuli za maendeleo ya wanawake na watoto.

### **3.0 HUDUMA ZINAZOTOLEWA KATIKA IDARA YA ELIMU MSINGI**

- I. Kusajili vikundi vya uzalishaji mali
- II. Kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vikundi
- III. Kuhamasisha jamii kujiunga katika vikundi vidogovidogo na kushiriki katika shughuli za maendeleo
- IV. Kujengea uwezo viongozi wa kata na vijiji juu ya masuala ya kijinsia
- V. Kutoa elimu ya mfuko wa afya ya Jamii (CHF)
- VI. Kuratibu zoezi la utoaji mikopo kwa vijana na wanawake

### **5.0 MATARAJIO YA IDARA**

Idara ya maendeleo ya jamii inatarajia kutoa mikopo kwa vikundi vya uzalishaji mali vya wanawake na vijana kwa mwaka huu wa fedha.

### **KARIBUNI WANANCHI KATIKA IDARA YA MAENDELEO YA JAMII**